**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule: 0756075291/0627032287**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0768876106/0629619421**
**Mwalimu wa Taaluma: 0742304100**
**Patron: 0754408615**

**Shule ya Sekondari Isingiro**

**S.L.P 167**

KYERWA

**Tarehe 08.04.2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi..........................................................................**
**S.L.P …........................**
**.........................………………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ISINGIRO HALMASHAURI YA KYERWA MKOA KAGERA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya HGK. Ni shule ya wavulana tu kwa kidato cha Tano.

Shule ya Sekondari Isingiro iliyopo katika Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Kyerwa, ipo upande wa kaskazini magharibi umbali wa km 13 kutoka makao makuu ya wilaya ya Kyerwa, upande wa kusini mashariki km 6 kutoka mji mdogo wa Isingiro, upande wa kusini magharibi km 85 kutoka mji wa

Kayanga kwa kupitia barabara ya Omurushaka -Nkwenda. Usafiri unaopatikana kutoka maeneo tajwa hapo juu ni wa magari madogo ya abiria (Hiace).

Ukitokea Manispaa ya Bukoba unaweza kupanda Bus la moja kwa moja kutoka Bukoba hadi Kyerwa utashuka Isingiro sekondari (shule ipo karibu na barabara) kwa nauli ya Tshs 14,000/= au unaweza kupanda Usafiri wa Hiace kutoka Manispaa ya Bukoba hadi Omurushaka (Nauli tshs 7,000/=) tena ukapanda usafiri wa Hiace za kutoka Omurushaka hadi Kaisho ambapo utashuka Isingiro sekondari (Nauli Tshs 7,000/=).

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14.08.2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13.08.2023.Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31.08.2023. mwanafunzi aje ana karatasi ya matokeo (result slip)

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

(i) Suruali 2 nyeusi zenye heshima, mfuko mmoja wa nyuma na miwili pembeni; suruali iwe na miguu yenye “turnups” isiwe “Modal style” (Tutazikagua kabla ya kumpokea).
(ii) Shati mbili nyeupe aina ya tetron mikono mirefu na tai yenye michilizi nyeupe na nyeusi
(iii) Viatu vyeusi (Ngozi ) jozi moja vinavyofungwa kwa kamba za viatu, vyenye kisigino kifupi
(iv) Soksi nyeusi jozi mbili)
(v) Mkanda mweusi wa suruali usiopungua na usiozidi inchi moja na nusu
(vi) Sweta ya shule yenye rangi ya kijani kijivu isiyo na mikono (kizibao)
(vii) Sare za michezo ni Bukta moja rangi nyekundu, T-shirt moja rangi ya njano, Viatu aina ya raba jozi moja, Soksi ndefu za michezo na Tracksuit rangi nyekundu

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Mahitaji ya kitaaluma ni Daftri kubwa 12 (counter book 4 quire), Kalamu za wino za kutosha, Penseli 3, Rula 1, Faili – Box file moja, Mkebe 1 wa hesabu (Set), Ream mbili za karatasi A4 (kwa mwaka), Daftari ndogo 10 za kufanyia mazoezi ya darasani,Mwanafunzi anashauriwa kuwa na vitabu vya tahasusi husika atakayosoma (orodha imeambatanishwa)

ii. vifaa vya usafi: Mwanafunzi aje na vifaa vya usafi wa majengo na mazingira ya shule ambavyo ni: Ndoo 1 ya lita 20 rangi yoyote, Jembe 1 na mpini, panga moja imara, Mfagio 1wa nje aina ya chelewa na karatasi 6 za chooni (Toilet papers) , mopper 1na soft broom 1

**iii.** Mahitaji ya bwenini ni kama ifuatavyo:

i. Suruali mbili damu ya mzee (zisizobana mwili –modo hazitakiwi) pamoja na T.shirt mbili rangi ya light bue zenye kola kwa ajili ya kuzivaa baada ya muda wa darasani na siku za Juma mosi na Juma pili.
ii. Godoro futi $2\frac{1}{2}$ x 6 na chandarua.
iii. Mashuka ( jozi 2) yenye rangi ya Bluu na Kijani, Blanketi (01) rangi yoyote, Mto na Foronya (Bluu au Kijani) na chanduluwa 1
iv. Sanduku imara la mbao au chuma lenye kufuli.
v. Sahani ya bati , bakuli, kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula
vi. Ndoo moja (lita 20) 1 kwa ajili kutunza maji na usafi binafsi, beseni 1 kwa ajili ya kuogea na na dumu la lita 5 la kuhifadhia maji ya kunywa
vii. Picha (passport size) 6; 2 za wazazi/ walezi, 2 za ndugu wa karibu na 2 za mwanafunzi na namba za simu za wazazi/walezi na ndugu 2 wa karibu .
viii. Sabuni za kutosha za kufulia na kuogea, Mswaki, Dawa ya Meno, Brashi na dawa ya kung'arisha viatu Vyeusi na mafuta ya kujipaka
ix. Mwamvuri (01), Tochi 1 na betri zake
x. Taulo (01) rangi yoyote, Ndala/Kandambili au Yebo pair (01).
xi. Mwanafunzi asipewe fedha nyingi, apewe fedha kidogo ya kujikimu na kununua mahitaji muhimu kama daftari pale inapobidi kufanya hivyo.

NB. **Mwanafunzi yeyote hataruhusiwa kuwa na nguo nyingine tofauti na sare za shule zilizoelekezwa hapo juu isipokuwa kwa maelekezo maalum ya daktari.**

## 2.3 Michango mbalimbali

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Malipo haya yalipwe akaunti ya shule namba 31901100051. Jina la akaunti: REVENUE COLLECTION A/C, ISINGIRO SE.**

## 3.0 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;
- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).
- ❖ Mwanafunzi aje na bima ya afya kwa ajili ya matibabu yake. Shule haitoi matibabu yoyote kwa mwanafunzi. Huduma ya matibabu ni jukumu la mzazi.

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4.0 Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya kukubali na kutii sheria za shule
ii. Taarifa binafsi za mwanafunzi;
iii. Hati ya uthibitisho wa tabibu
iv. Orodha ya vitabu

**6.0** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**.....................................................**

**EUSTACE G. MPILI**

**MKUU WA SHULE**

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. **TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

**Mkuu wa shule: EUSTACE G.MPILI 0756075291/0627032287**
**Makamu Mkuu wa Shule: MJUNGU S.B MATETE: 0768876106/0629619421**
**Patron1: EVARISTER SIMBA PASTORY: 0754408615/0621217751**

**Patron 2: SHWAIBU ISSA MUGUHA : 0621861896**

**SHULE YA SEKONDARI ISINGIRO**
**KIAMBATANISHO “A”**
**FOMU YA KUKUBALI NA KUTII SHERIA ZA SHULE**

Mimi………………………………………………………………………………(jina la mwanafunzi) nimepokea barua ya kuingia kidato cha tano katika shule ya sekondari Isingiro. Nakubali nafasi hiyo kwa moyo mkunjufu. Baada ya kusoma na kuelewa sheria za shule, naahidi kuwa nitatii sheria hizo kama zilivyoainishwa katika fomu ya maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari Isingiro. Endapo nitashindwa kutii sheria hizo hatua inayostahili ichukuliwe dhidi yangu

Natoa ahadi hii mbele ya Mzazi /mlezi wangu ambaye ametia sahihi yake hapa chini.

Jina la mwanafunzi ………………………………….…sahihi……………………….Tarehe…….……

Mimi………………………………………………..(Jina la mzazi /mlezi) ambaye ni mzazi /mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu, nakubali mwanangu ajiunge kidato cha tano katika shule ya sekondari Isingiro na kutii sheria za shule na naahidi kushirikiana na Uongozi wa shule ili kuhakikisha tunatoa malezi bora kulingana na sheria hizo na nyingine ambazo hazikutajwa pia.

Iwapo sitakuwepo mimi likitokea tatizo ninaweza kuwakilishwa na

1. ………………………………………………….ambaye ni ……………………………………..

2. …………………………………………...…….. ambaye ni ……………………………………..
(Eleza uhusiano wako na wawakilishi hao)
Jina la mzazi / mlezi ……………………………………………
Sahihi ….……………………………………………………….

Tarehe………………………………………………………

KUHUSU MWANAFUNZI KUTOMILIKI SIMU SHULENI.
Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu shuleni. Mwanafunzi akibainika kumiliki simu shuleni adhabu zifuatazo kwa mwanafunzi huyo zitatolewa:-

i. Kuchapwa viboko vinne 4 mbele ya wanafunzi wote mstarini
ii. Kusimamishwa masomo siku 21.
iii. Siku ya kurudi shuleni mwanafunzi atatakiwa kuja na mzazi/mlezi wake na faini ya kulipia gharama za uharibufu wa miundombinu ya umeme kutokana na kuchaji simu kwa siri kwa kutmia miundombinu hiyo. Faini itatokana na maamuzi yatakayotolewa na bodi ya shule. Endapo mzazi/mlezi atashindwa kutekeleza vipengele tajwa (i-iv) mwanafunzi atafukuzwa shule kanma ilivyoelezwa katika sheria za shule kifungu no. 3.2 (xv).

KIAPO CHA MWANAFUNZI KUTOMILIKI SIMU WALA VIFAA VYA SIMU.
Mimi (jina la mwanafunzi)………………………………………………………… kwa hiari yangu na nikiwa na siha njema ya akili naapa kwamba sitomiliki simu ya aina yoyote wakati wote wa masomo yangu ya kidato cha tano na sita . Ikiwa nitakiuka kiapo changu hiki sheria ya Elimu Na 25 ya 1978 itumike dhidi yangu. Pia ninaahidi kutovunja sheria , kanuni na taratibu za shule na za Taifa langu kwa ujumla.
JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………………………..
SAHIHI………………………
TAREHE……………………………………………………………………………..

# SHULE YA SEKONDRI ISINGIRO

## KIAMBATANISHO B

**TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI;**

i. Jina la mwanafunzi ……………………………………………………. jinsi…………………… Tarehe ya kuzaliwa…………………
ii. Shule ya Sekondari aliyotoka……………………………………………………………………………………………………
iii. Jina la baba…………………………………………......... kazi yake……………………………. Na.ya simu………………………………..
iv. Jina la mama……………………………………………kazi yake……………………………… Na. ya simu………………………………..
v. Kijiji /mtaa wanapoishi………………………………………………. Wilaya……………………………mkoa ………………………….
vi. Dini…………………………………………………………………..
vii. Majina ya ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kutoa msaada pindi wanapohitajika
   a. ……………………………………………………………. Anakoishi…………………………………… Na. ya simu…………………..
   b. ……………………………………………………………. Anakoishi…………………………………… Na. ya simu…………………
   c. ……………………………………………………………. Anakoishi…………………………………… Na. ya simu…………………
   d. ……………………………………………………………. Anakoishi…………………………………… Na. ya simu…………………
viii. Michezo anayoweza kushiriki mwanafunzi shuleni
   ……………………………………………………………… …………………………………………………….. …………………………………….

NB: Je wazazi wote wako hai ? . Ndiyo/ Hapana (Kata isiyositahili)
Kama amefariki /wamefariki aliyefariki ni…………………………………………………………………………………………………….

**KUKUBALI NA KUTII SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE**.

Mimi (jina la mwanafunzi)…………………………………………………………………….naahidi sitashiriki kabisa katika fujo/migomo na kutenda makosa ya jinai shuleni na maeneo mengine .Pia naahidi kuzifuata taratibu na sheria zote za shule kwa faida yangu binafsi, shule na Taifa kwa ujumla .Endapo nitakwenda kinyume na taratibu na kanuni za shule nakubali kufukuzwa shule, kusimamishwa masomo na kufikishwa mahakamani au kupewa adhabu nyingine kulingana na sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 na au sheria ya makosa ya jinai ya mwaka 2002

JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………… SAINI……………………………………TAREHE………………
JINA LA MZAZI/MLEZI……………………………………………………..SAINI……………………………………TAREHE………………..

**MZAZI/MLEZI KUKUBALI KUSHRIKIANA NA SHULE KATIKA MALEZI YA MTOTO WAKE.**

Mimi (Jina la mzazi/mlezi)……………………………………………………. nakubaliana na sheria , kanuni, kulipa ada na michango yote kwa wakati muafaka na kutekeleza maelekezo yatolewayo na shule. Vilevile , naahidi kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwa uongozi wa shule pindi nikihitajika kuhusu tabia, mwenedo au suala jingine lolote linalomhusu mtoto wangu na maendeleo ya shule kwa ujumla.

JINA LA MZAZI/MLEZI…………………………………………………………… SAINI…………………………..TAREHE……………

**SHULE YA SEKONDARI** ISINGIRO

## KIAMBATANISHO C

## HATI YA UTHIBITISHO WA TABIBU (anayetambuliwa na serikali)

Nathibitisha kwamba nimemchunguza mwanafunzi

Jina…………………………………………………………………………………………………

Kinyesi…………………………………………………..Matokeo……………………………………
Mkojo…………………………………………………Matokeo……………………………………
Macho…………………………………………………Matokeo……………………………………
Damu………………………………………………… Matokeo……………………………………...
Masikio ………………………………………………  Matokeo…………………………………...
T.B……………………………………………………  Matokeo……………………………………...
Mapigo ya moyo…………………………………… ...Matokeo………………………………………
Vipimo vinginevyo:
……………………………………..................................................................................
........................................................................................................................................................
........................................................................................................................................................
........

**MATIBABU** yafuatayo yametolewa (kama ni ugonjwa wa kudumu eleza)
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………

Jina la tabibu………………………………………………

Wadhifa………………………………………………..

Kituo cha kazi na hadhi yake………………………………………..

Sahihi……………………………………………………..…

Tarehe………………………………………………………..

Muhuri ………………………………………………

**SHULE YA SEKONDARI ISINGIRO**

**KIAMBATANISHO "D"**

**ORODHA YA VITABU**

| SUBJECT | BOOK TITLE |
|---|---|
| HISTORY | 1. How Europe underdeveloped Africa - By Walter Rodney |
| | 2. General History of Africa - By AssaOkot |
| | 3. Contemporary Historical Events - Vol. I & II By Shibitali C. K Tumaini |
| | 4. The Revolutionary Years, West Africa Since 1800 - By Webster J. B & Boachen A. A |
| | 5. Mastering Modern World History. - By Norman Lowe |
| FASIHI | 1. Nadharia ya Fasihi Kidato cha Tano na Sita – Masebo – Oxford university Press |
| USHAIRI | 1. Haji, G, H. (1994). Kimbunga; Dar es Salaam. TUKI |
| | 2. Khatibu, M (1988). Fungate ya Uhuru;Dar es Salaam. Dar es Salaam University Press. |
| | 3. Mvungi, (1985). Chungu Tamu; Dar es Salaam. Tanzania Publishing House. |
| | 4. H. J. Mwansoko Kitangulizi cha Tafsiri Nadharia na Isimu |
| | 5. Rboert S. (1970); Mapenzi Bora, Dsm; Evance & Brothers LTD |
| TAMTHILIA | 1. Hussein , E. (1988). Kwenye Ukingo wa Thim;Nairobi Oxford University Press. |
| | 2. Mbogo, E (1993). Morani; Dar es Slaam. Dar es Salaam University Press |
| | 3. Mohamed, S. A (1990). Kivuli Kinaishi;Nairobi Oxford Univestriy Press |
| | 4. Penina Mhando; Nguzo Mama |
| RIWAYA | 1. Msokile, M (1990). Usiku Utakapokwisha; Dar es Salaam: Dar es Salaam Univesity Press. |
| | 2. Robert, S (1967). Kufikirika; Nairobi Oxford Univesity Press |
| | 3. Shafi, A.S. (1997). Vuta n'Kuvute; Dar es Salam. Oxford University Press |
| | 4. Tuwa, H (2007). Mfadhili; Dar es Slaam. Macmillan. |
| LUGHA NA SARUFI | 1. Kiswahili. Kidato cha tano na sita (2012) James J & Faustino M |
| | 2. Nadharia ya lugha ya Kiswahili1: Kidato cha Tano na Sita – Nyambari Nyangwine na Masebo (2010) |

| | |
|---|---|
| | 3. Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la pili: English – Swahili Dictionary – TUKI |
| GEOGRAPGY | 1. Pritchard M, John (1971) Practical Geography for Africa |
| | 2. PT. Msabila (2007) A Compressive Approach to Physical Geography for Secondary Schools. |
| | 3. Msabila, DT (2000) An Integrated Focal Regional Study on Human and Economic Geography. |
| GENERAL STUDIES | 1. General Studies For Secondary School - By Mbalase, R. |
| | 2. Bigirwamungu, J. & Deogratius S.M (2012) Understanding Advanced Level General Studies: Advanced Level Secondary Schools, |
| | 3. Nyangwine, C.M, Bukagile G.R & Maluka S.O (2010) Contemporary Approach for Advanced Level: General Studies Notes form 5 & 6. |
| | 4. General Studies By SETA |
| | 5. General Studies, Supplementary Book for Advanced level and Colleges , Second Edition – Konrad<br>Adenaker Stiftung |